# Uamilifu wa Taashira katika Tamthilia za *Zilizala* na *Sudana*

*Waithiru Kago, Wendo Nabea* na *James Ogola Onyango*
*Chuo Kikuu cha Laikipia*

**Ikisiri**

**Makala haya yanahusu matumizi na uamilifu wa taashira katika tamthilia za Zilizala na Sudana. Katika makala haya matumizi ya taashira yalichunguzwa kupitia vyombo vya usafiri, hali za kimaumbile na miundomsingi. Makala haya yaliyojikita katika nadharia ya baada ya ukoloni yanaonyesha kuwa taashira imetumika katika tamthilia zilizopo kama mbinu ya kusana mambo yanayoathiri kitovu cha jamii. Haya ni pamoja na viongozi wa kiimla, ufisadi, ukabila na ubinafsi. Aidha, yanaeleza kuwa taashira imetumika vyema katika tamthilia hizi madhali imesaidia waandishi kuepuka uwezekano wa kusawiri masuala yanayokumba jamii paruwanja, jambo ambalo lingenyima kazi zenyewe mvuto. Badala yake imeonyeshwa kuwa waandishi walifinyanga lugha na kuyasawiri masuala ya kawaida kwa namna ngeni na ya kutendesa kupitia taashira. Yanadhihirisha tadi na inda zinazotumiwa na baadhi ya watawala katika mataifa yanayoinuka kiuchumi kujinufaisha kibinafsi pamoja na vikaragosi wao. Isitoshe, makala haya yamedhihirisha jinsi viongozi wa mataifa hayo hudhibitiwa na watawala katika mataifa yaliyoinuka kiuchumi na kusababisha ufukara wa raia katika mahusiano yanayofichika katika istilahi ya kitasfida ya utandawazi.**

**Maneno Muhimu:** Taashira, Miundomsingi, Watawala, Vikaragosi, Utandawazi

**Utangulizi**

Kama kazi nyinginezo za fasihi, tamthilia hutungwa ili kutimiza malengo fulani. Malengo haya ndiyo humfanya mtunzi achague mbinu atakazotumia huku akiacha mbinu nyingine. Mbinu ni vipengele vya kimtindo na kimuundo ambavyo hupatikana katika kazi yoyote ya kifasihi (Wamitila 2003). Kwa mfano, tamthilia za *Zilizala* (Kimani Njogu) na *Sudana* (Kimani Njogu na Alamini Mazrui) zimetumia mbinu ya taashira pakubwa. Taashira ni aina ya tamathali ya usemi ambapo jina la sehemu ya kitu hutumiwa kuwakilisha kitu kamili au kingine kinachohusiana nacho. Neno au jina kuchukua nafasi ya neno au jina lingine linalohusishwa nalo. Ni mbinu ambayo hutumiwa na baadhi ya waandishi kuashiria dhana zinazokanganya, hisia pamoja na hali za kiakili. Kulingana na Wamitila (2003: 208): taashira ni aina ya tamathali ya usemi ambapo jina la sehemu ya kitu hutumiwa kuwakilisha kitu kamili au kingine kinachohusiana nacho.

Tamthilia ya *Zilizala* inaangaza masuala mbalimbali ya kijamii kitaashira. Mathalani, anwani ya *Zilizala* inaashiria kuhamishwa kwa wananchi kwa lengo la

kutwaa ardhi yao, vipigo, ukoloni, dharau la viongozi kwa wananchi na mabadiliko. Mojawapo ya sanaa zinazofanikisha kazi hii ni mbinu ya taashira. Sababu kuu ya kutumia taashira ikiwa kwa sababu ni fasihi ambapo ni ulimwengu uliotungwa lakini si halisi. Masuala yaliyowasilishwa yanaweza kuibua hisia kali na hivyo mwandishi anatumia taashira kama leseni ya lugha. Mathalani, Timika ni taashira ya gereza ambalo hufungiwa wazalendo wanaozalisha mapinduzi katika mataifa mbalimbali ya Kiafrika. Pia ili kuficha kasumba kwa kutumia taashira kama nyenzo za kuzungumza baina ya wahusika, kumulika uozo, uonevu na hila au ubaya katika jamii.

Kimwavuli, *Zilizala* inahusu Udenda ambaye kwanza anachaguliwa diwani wa Kusudi kabla ya kufanywa Meya. Akiwa katika chuo kikuu alikuwa mtetezi wa wanyonge na hivyo watu wanamchagua wakiwa na matumaini mengi kumhusu. Lakini anaanza kuwanyanyasa maskini hawa kwa ajili ya tumbo lake binafsi. Anafanya hivi kwa kushirikiana na mabwanyenye wa mataifa ya kigeni. Anadhulumu watu kwa kuwahamisha makwao kwa kisingizio cha zilizala ilhali nia yake ni kujinufaisha binafsi na pia kunufaisha mabepari kutoka mataifa ya nje. Hatimaye watu hasa vijana na kina mama wanaungana na kumtia mbaraoni kama namna ya kujinusuru.

Katika tamthilia ya *Sudana*, watunzi wanaangaza ukoloni mamboleo. Katika shairi tangulizi, watunzi wanaeleza jinsi Wazanji walipigania uhuru ambao hatimaye uligeuka ndoto. Meli ya Wazanji inayoabiri baharini inakumbwa na matatizo ya kiufundi na kuhatarisha maisha ya abiria. Ufuoni, wanaona Wamerope na kuomba msaada kutoka kwao. Wamerope wanawarushia kamba wanazofunga katika mashua na kuvutwa na Wamerope hadi ukingoni. Kumbe hisani ya Wamerope ni uzandiki? Punde, Wazanji wanaanza kufanyishwa kazi ngumu na Wamerope. Kadhalika, mashua yao inabomolewa na mbao zake kutumiwa kukarabati mashua ya Amerope iliyochakaa. Kitaashira bara la Afrika lanyonywa na mataifa ya Marekani na Uropa. Waandishi wanaashiria changamoto ambazo Waafrika hukumbana nazo katika harakati za kupigania uhuru na kulilinda bara la Afrika dhidi ya unajisi wa mataifa ya Uropa na Marekani. Mateso wanayoshindiliwa Wazanji ni ya uchungu ikiwemo kuwekwa vifungoni, kuchapwa, kukatwa viungo vya miili na kubakwa. Hatimaye Wazanji wanapanga njama na kuanzisha vita vya ukombozi dhidi ya Wamerope ambapo damu nyingi inamwagika, ya wadhalimu kwa wadhulumiwa.

**Matumizi ya Taashira**

Watunzi wa fasihi ni wasanii ambao hutumia mitindo mbalimbali kufaulisha tungo zao (Wamitila 2002, 2003, 2010; Mbatiah 2001). Kulingana na Ntarangwi (2004), Njogu na Chimerah (1999) na Syambo na Mazrui (1992), watunzi hufinyanga lugha na kuibuka na mitindo mbalimbali katika kazi zao. Mojawapo ya mbinu zinazotumiwa kama mtindo katika fasihi ni taashira. King'ora (2014), Kilanga (2014) na Too (2011) ni baadhi ya wasomi ambao wamefasili dhana taashira.

Wanaafikiana kuwa taashira inaweza ikawa kitu au mfano wa kitu kinachowakilisha kitu kingine au kiumbe kisichoonekana kama vile shetani, mungu, malaika na kadhalika. Hivyo, taashira hupatia kitu, jambo, mtu, hali, hisia au mnyama maana iliyo na uketo. Isitoshe, inaweza kupanua maana ya kawaida mpaka ikapata maana tofauti kabisa. Ikizingatiwa kuwa hugeuza masuala ya kawaida na kuonekana kama mambo mapya, ni muhimu kutalii kazi zilizopo kubaini jinsi uongozi na utandawazi husawiriwa katika kigezo cha taashira.

Katika ujenzi wa taashira, waandishi hurejelea vitu, watu, wanyama na hali na kuzifinyanga ili ziwakilishe vitu, watu, wanyama au hali nyingine. Hufanya hivyo wakiwa na matlaba tofautitofauti mintarafu ya maudhui wanayosuka. Onyango (2011) akimnukulu Khamis 2014) anabainisha viambajengo kadhaa vinavyoweza kutumiwa kujenga taashira katika tungo za fasihi. Kauli yake ina mashiko kwa kuwa waandishi wa *Zilizala* na *Sudana* walizingatia viungo kadha wa kadha kujenga taashira. Hivi ni pamoja na vyombo mbalimbali, majengo na hali za kimaumbile. Wametumia vipashio hivi kitaashira na kuibua maana tofauti na ile iliyozoeleka katika maisha ya kila siku. Utafiti ulibaini kuwa waandishi hawa wametumia taashira kusawiri masuala nyeti katika jamii. Wameitumia kuangaza masuala mazito kuhusu uongozi na utandawazi hasa katika mataifa ya kisasa.

**Taashira ya Vyombo vya Usafiri**

Katika *Zilizala*, mwandishi ametumia matatu, yaani basi dogo linalobeba abiria. Matatu hii inaitwa Kifaduro. Kifaduro kwa kawaida ni ugonjwa wa kukohoa ambao watu wanaweza kuambukizana. Mwandishi ametumia matatu hii kama taashira ya chama cha kisiasa. Ni chama ambacho kina sera mbovu zinazosababisha maangamizi na si ajabu kinaitwa kifaduro. Hivyo, basi la kifaduro ni ishara ya chama cha kisiasa kilicho na maradhi. Maradhi yenyewe ni ufisadi. Ni chama kinachojali maslahi ya waliojiweza kiuchumi na kuwapuuzilia mbali wasiojiweza. Kwa mfano, mhusika Udenda anasema, "Haya! Haya! Mwenye nguvu mpishe; la sivyo, utafagiliwa! Amkeni jamani, wakati umefika wa virago kuvifunganya. Haya! Haya! Matatu ya Kifaduro yaondoka jamani … (uk. 5).

Isitoshe, matatu ya kifaduro, yaani chama hicho cha kisiasa, ni chanzo cha kifo cha kizazi na taifa kwa jumla. Hii ni kwa sababu babu na bibi ambao ni chanzo cha vijana hawana nafasi katika ulimwengu wa jamii ya Rutuba. Kiongozi wao Udenda anashikilia kuwa, *Forwards Ever Backwards Never!* Babu na Bibi wanadaiwa kuishi jana ilhali Udenda anadai wao ni watu wa kisasa. Udenda anaashiria viongozi wengi wa mataifa ya Kiafrika ambao huangamiza kiini cha vizazi.

Chama hicho cha kisiasa kinachoashiriwa na matatu ya kifaduro hali kadhalika ni chanzo cha ukosefu wa usalama. Wanaoingia ndani ya matatu wanahatarishiwa maisha yao kwa kuzungushwa kila mahali. Angela, mkewe Udenda, hakika anahofia maisha ya abiria waliopanda matatu yenyewe. Matatu hii pia hutumiwa kama kipimajoto na wanasiasa kupimia umaarufu. Baada ya kutambua kuwa kile chama hakina umaarufu wa kutosha kuwavusha hadi kwenye ubwanyenye, wao

hukivunja na kubuni kingine kinachoafiki tamaa yao, tayari kwa uchaguzi utakaofuata. Mathalani, katika mataifa mengi barani Afrika, tukio hili ni la kawaida kiasi cha kuonekana kama jambo sawa. Baadhi ya viongozi hutumia vyama tofauti vya kisiasa kuwapumbaza watawaliwa wakati wa uchaguzi kabla ya kuwanyanyasa wanapopata mamlaka.

Vilevile mtunzi ametumia chombo cha trekta kama taashira. Trekta ni chombo chenye injini kinachoendeshwa kama gari ambacho hutumika kulima au kuzolea vitu. Aidha, trekta huweza kutumika kubebea mizigo au hata kuvuruta magogo makubwa. Katika *Zilizala,* trekta ni taashira ya viongozi mabaradhuli katika mataifa mengi barani Afrika. Lao kuu ni kuangamiza wananchi kwa nia ya kutwaa mashamba yao. Mshahara duni wanaolipwa vijana na wafanyakazi wa mji wa Rutuba kwa mfano, unaonesha chumi zilizozorota katika mataifa mengi yanayoinuka kutokana na unyanyasaji, mateso na maonevu ya viongozi. Ni viongozi waoga wasio na ujasiri wa kujitokeza hadharani. Mathalani, Udenda anasema:

> Haya basi, wahini! *(Anachukua simu yake kutoka mfukoni; anapiga upesiupesi huku akighadhibika isipoingia.)* Halo! *Come on!* Udenda hapa … Watu wameanza kutoka nyumbani mwao … Sawa! Wekeni trekta na kila kitu tayari … na mafundi pia wakae tayari! *(Kwa hasira.) Shut up!* Nitakwambia nikiwa tayari …Weka trekta ishirini tayari hapo karibu na Jitochafu. Ficha karibu na kichaka ili watu wasione. Unasikia? (uk 6).

Haya yanadhihirisha jinsi viongozi waovu huwalaghai wananchi msimu wa kampeini na kuwapatia ahadi nyingi nzuri ila huwa hazitimizwi. Wao huficha nia yao halisi hadi baada ya kuchaguliwa ambapo ukweli hujiweka bayana mchana peupe.

Katika *Sudana*, Kimani Njogu na Alamin Mazrui wametumia chombo cha bahari ambacho ni mashua. Mashua ni chombo ambacho huendeshwa kwa makasia, tanga au injini. Mashua huweza kusafirisha watu pamoja na mizigo ya aina mbalimbali. Ili kufanikisha usafirishaji huu, chombo hiki hupitia kwenye maji hususan ya bahari au ziwa. Katika *Sudana*, Kimani Njogu na Alamin Mazrui wametumia neno mashua kitaashira. Mathalani, pana mashua ya Amerope ambayo ni taashira ya mataifa tajiri ya Uropa na Marekani. Jina Amerope limeundwa kutokana na kuunganishwa kwa sehemu za majina mawili; Amerika na Uropa. Uropa ni jina lingine la Ulaya. Mhusika Amerigo anayesimamia Amerope ni ishara ya viongozi wa mataifa tajiri ya Uropa na Marekani, ambao ni dhalimu.

Katika mashua hii Amerigo ni nahodha. Unahodha wake wa mashua Amerope unaashiria uongozi. Nahodha ni taashira ya viongozi dhalimu wa mataifa ya Amerika na Uropa ambao wanakuza chumi zao kwa kunyanyasa mataifa yanayoinuka jinsi tu mashua ya Wazanji inang'olewa mbao kukarabati mashua ya Amerope. Vilevile pana mashua ya Zinji. Zinji ni neno linalotokana na neno zanji

linalomaanisha weusi. Hivyo, mashua ya Zinji ni taashira ya mataifa ya watu weusi waliopo Afrika.

Kwa jumla mashua ni taashira ya mabara na kadhalika mataifa mbalimbali ulimwenguni. Mashua hizi zinaabiri baharini yaani duniani, kama ilivyokwisha tajwa. Katika bahari hii, waandishi wanatusawiria mabara matatu kupitia taashira ya mashua: Bara la Zinji, yaani la watu weusi na mabara ya Amerope yaani Amerika na Uropa. Mashua hizi ni muhimu madhali ndizo zinatusawiria mahusiano kati ya mataifa ya bara la Afrika na yale ya mataifa ya Uropa na Marekani. Mashua ya Zinji inakumbwa na matatizo ya kiufundi na inabidi iopolewe baharini kwa msaada wa Wamerope. Lakini ni msaada wa kinafiki maadamu muda si muda, mbao za mashua ya Zinji zinang'olewa kukarabati mashua ya Amerope ambayo imechakaa. Huu bila shaka ni unyanyasaji unaoakisi namna mataifa ya Kiafrika yanavyohujumiwa na baadhi ya mataifa yenye nguvu kupitia tasfida ya utandawazi.

Mashua huwa na vifaa vingine vingi ambavyo huweza kutumika wakati wa dharura, kama vile kamba na hori. Kamba inayotumika kuwasaidia Wazanji kuwavusha kutoka kwenye mashua ya Zinji hadi ile ya Amerope ni taashira ya unyanyasaji katika utandawazi. Mataifa yenye nguvu ulimwenguni yanalaghai mataifa yanayoinuka kuwa yatawafaidi lakini mwishowe yanawanyanyasa. Ulaghai huu unadhihirika wakati Amerigo anasema haya:

> Haya, wamefika karibu; watupieni kamba. Kamba! Kamba! Kamba! *(Mabaharia wachache wanasogea mbele na kurusha kamba kupitia mlango mmoja wa jukwaa)* Na ile mashua yao ifunganishe na yetu. *(Mabaharia wengine wanatoka haraka haraka.)* Ni Wazanji wale … na … na mwanamke, pia mna mwanamke ndani. (uk12).

Nahodha wa mashua ya Amerope Amerigo ana jina la kitaashira. Jina hili limetokana na majina mawili Ameri na go. Ameri ni silabi za mwanzo za neno Amerika ilhali *go* ni neno la Kiingereza linalomaanisha kwenda. Lakini jina Ameri linapotamkwa linawiana na *merry* la Kiingereza linalomaanisha furaha. Katika Kiingereza kuna shughuli ya wanachama kuchangiana fedha kwa ajili ya kufaidi mmoja wao yaani *merry go round*. Yamkinika watunzi wametumia jina Amerigo kulenga si Amerika pekee kama nchi, bali ulaghai unaoendeshwa na mataifa yenye nguvu katika utandawazi wakijifanya kushirki *merry go round* na mataifa yanayoinuka kiuchumi mathalani yale ya Afrika. Hivyo, nahodha Amerigo ni laghai ambaye yupo radhi kunyanyasa Wazanji wanaotoka ndani ya mashua ya Zinji kwa ajili ya kunufaisha mashua ya Amerope yaani mataifa ya Uropa na Marekani.

Si ajabu mashua ya Zinji inaondolewa mbao zinazotumika kukarabati mashua ya Amerope ambayo ina mbao zilizochakaa. Amerigo anatumia hila anapodai kuwa mashua ya Amerope imefaulu kuokoa watu wengi kama vile kina Sudzungu, Sudana, Shume na Sizwe, lakini ukweli ni kuwa wanageuzwa watumwa wa kushona viraka, kufanya kazi za sulubu na kupigwa ovyo kwa maonevu tu.

Mbao zilizong'olewa kutoka mashua ya Zinji ili zitumike kuirekebisha mashua ya Amerope ni taashira ya ufyonzaji wa rasilmali unaoendelezwa na mataifa ya ulimwengu wa kwanza dhidi ya mataifa fukara ya Kiafrika kiuchumi, kisiasa, kielimu na kijamii. Hili limegubikwa na tasfida ya istilahi ya utandawazi ambapo mataifa yanadaiwa kukaribiana au kuja pamoja kufaana kiuchumi, kisiasa na hata kibinadamu. Misumeno ya kukata mbao hizo ni taashira ya ala zinazotumiwa na mataifa tajiri ya Marekani na Uropa kuponza mataifa mengi hasa Afrika, hususan kiuchumi na kijamii. Kukatwa na kuvunjwa kwa mbao za Zinji ni taashira ya uharibifu na ufyonzaji wa mataifa ya bara la Afrika na viongozi wa mataifa yenye nguvu.

**Taashira ya Hali za Maumbile**

Hali za maumbile huwa anuwai. Mojawapo ya taashira za kimaumbile zinazotumika katika *Zilizala* ni udongo. Udongo ni sehemu ya juu ya ardhi ambayo ni laini na ambapo mimea huweza kuota. Pia ni mchanga unaotumiwa na mfinyanzi kufinyanga bidhaa mbalimbali. Aina ya udongo ulio katika sehemu za Afrika ni taashira ya aina za viongozi walio katika mataifa mengi barani Afrika. Viongozi hawa hawana msimamo na si wazalendo. Wanaupanda na kuupalilia uongozi mbaya katika udongo. Mama anamwambia Udenda kuwa mjukuu wake Atieno, anayesoma chuo kikuu anakusudia kufanya utafiti kuhusu mitetemko ya ardhi katika mataifa ya Afrika. Mitetemeko hii ni hatari kwa kuwa hupasua mianya ardhini ambapo udongo husonga na kusababisha maangamizi na hasara kubwa. Atieno anakisia mitetemeko hii inasababishwa na udongo uliopo katika mataifa ya Afrika.

Mtetemeko wa ardhi bila shaka ni taashira ya mapinduzi ambayo yamekuwa yakitokea katika mataifa ya Afrika mara kwa mara. Hakika mapinduzi haya husababisha vifo na hasara kubwa. Inadaiwa kuwa udongo huu ni mwekundu na huvuta radi. Kadhalika udongo wenyewe ni telezi na unakosa umadhubuti. Udongo mwekundu ni taashira ya viongozi ambao ni vikaragosi wa watu wa mataifa ya kigeni ambao aghalabu huwa na ngozi nyekundu. Ikizingatiwa viongozi wa mataifa ya Kiafrika wanaweka maisha ya mataifa yao rehani kwa ajili ya watu wekundu, si ajabu udongo unasemekana kuwa ni mwekundu. Ni udongo usioambatana na udongo wa Waafrika ambao bila shaka unapaswa kuwa mweusi.

Mbali na hayo, udongo ni taashira ya viongozi Waafrika. Wananasibishwa na udongo mwekundu, wenye utelezi na usio madhubuti kudhihirisha udhoofu wao. Hawana msimamo na hawawezi kufanya uamuzi wowote bila ya kuogopa kukashifiwa na mataifa tajiri ya Ulaya. Wao hujali maoni ya viongozi wa Ulaya na Marekani kuliko wanavyojali kwikwi na malalamishi ya wananchi waliowachagua. Lao kubwa ni shibe na mamlaka. Ndiposa wengi hukatalia mamlakani, hata baada ya kushindwa kwenye uchaguzi au hata kuiba kura wakati mwingine.

Isitoshe, shamba limetumika kitaashira. Shamba ni kikataa ambapo watu huweza kulima ili wajiambulie riziki. Pia huweza kuwa janibu zilizo nje au mbali na mji.

Kwa kawaida, nomino shamba hurejelea ardhi iliyolimwa na kupandwa mazao. Katika *Zilizala*, shamba limetumika kama taashira ya mataifa yanayoinuka na yaliyo mbali na miji. Wakati huo huo, pana ulinganishi wa mashamba haya na miji ambayo ni mataifa yaliyoinuka kiuchumi kama vile Marekani na Ulaya. Hivyo, shamba ni taashira ya mataifa yenye chumi duni, kwa mfano, baadhi ya yale ya Afrika. Udongo unaorejelewa na Angela kama mkungu ni taashira ya uhuru unaotamaniwa katika mataifa mengi yanayonyanyaswa katika ukoloni mamboleo. Hata hivyo, ili kuupata uhuru, inawalazimu wale wanaonyanyaswa waupiganie.

Katika *Sudana*, pana ishara ya bahari kuashiria ulimwengu. Ni taashira ya dunia ambapo pana mataifa na mabara yaani, mashua mbalimbali. Katika bahari hii, pana wale wanaonyonya majasho ya wenzao. Kwa mfano, mashua ya Wazanji yamkini Waafrika, inapata matatizo ya kiufundi ikiwa inaabiri. Inabidi waliomo wasaidiwe na kina Amerigo waliokuwa na mashua ya Amerope, ambayo tayari imetia nanga ufuoni. Mtagusano huu unadhihirisha jinsi mataifa ya ulimwengu yanahusiana. Yale yaliyo taabani yananusuriwa na yale yenye uwezo jinsi tu mashua ya Zinji inanusuriwa na mashua ya Amerope. Haya yote yanaashiria jinsi mataifa yenye nguvu ulimwenguni husingizia kusaidia mataifa yanayoinuka kiuchumi japo ukweli ni mwingine. Mathalani, baada ya mashua ya Zinji kukumbwa na matatizo ya kiufundi, Wamerope wanajitolea kuipoa suala ambalo linaonekana kama hisani. Hata hivyo, baadaye wanang'oa mbao zake kukarabati mashua ya Amerope. Hivyo, bahari inaashiria ulimwengu ambapo mataifa mbalimbali yanaendeleza mahusiano, mengine yakiwa na mahusiano ya kitabaka ambapo mwenye nguvu anamnyonya maskini.

Aidha, kisiwa kimetumika kitaashira. Baada ya mashua ya Zinji kuopolewa, Amerigo anatazama kwenye upeo na kudai kuwa anaona kisiwa. Anasema kisiwa hicho kinampasha taashira ya kipusa. Kisiwa hiki ni taashira ya rasilmali za Waafrika ambazo wageni hutamani na wakati mwingine kunyakua kwa nguvu. Kwa mfano, Amerigo anadai kuwa angependa kuabiri baharini na huyo kipusa huku wakipanda na kushuka mawimbi. Suala hili linaashiria jinsi angependa kujuana kimwili na msichana huyu, ithibati zaidi kuhusu namna rasilmali za mataifa ya Kiafrika hunajisiwa na watu wa mataifa ya kigeni. Isitoshe, bara la Afrika na rasilmali zake linamithilishwa na msichana ambaye mwanamume, yaani mataifa ya Amerika na Uropa wangependa kulala naye. Hivyo, kisiwa hiki kinadhihirisha tamaa ya fisi ambayo mataifa ya kigeni yanayo kwa mataifa ya Afrika na rasilmali zake.

Kitendo cha unajisi katika *Sudana* kimetumika kitaashira. Unajisi huu unafanyika kwenye chumba kilichopo kando ya bahari. Kwa mfano, Amerigo anamfunga mama Sudana kwenye kitanda katika chumba chake na kumnajisi. Inabidi amnajisi akiwa amepoteza fahamu madhali Sudana ni mkali na awali amempiga Amerigo makofi na kumparura kwa kucha. Unajisi huu ni taashira ya ubadhirifu wa mali ya Waafrika na watu wa mataifa ya kimagharibi huku Waafrika wenyewe wakiachwa wakinyong'onyea katika ufukara. Unajisi huu unapelekea

kuzaliwa kwa mtoto Sudzungu. Sudzungu ana Usudani yaani, Uafrika na Uzungu. Mhusika huyu ni ishara ya kuhulutiana kwa utamaduni wa Kiafrika na Kizungu unaosababisha ukosefu wa utambulisho ambapo watu ni mithili ya popo ambaye si mnyama na si ndege. Hili ni jambo la kutia wasiwasi kwa kuwa mila na desturi za Kiafrika zinamomonyoka kutokana na maingiliano na watu wa kigeni. Cope na Kalantzis (2002) wanasisitiza kwamba ni utambulisho ambao hujenga utaifa wa watu, na hivyo iwapo watu wamekosa utambulisho, utaifa na ikizidi Uafrika wao, utakosekana pia. Lakini ikizingatiwa kuwa unajisi huu unasababishwa na Wamerope katika mataifa ya Kiafrika, yamkinika wao hawaathiriki kwa njia yoyote mbovu.

Pana mimea ambayo hukua kivyake na ile hupandwa na watu. Katika makala haya, mimea imechukuliwa kama mojawapo ya hali za kimaumbile. Mimea ni aina ya majani ambayo huota ardhini kutokana na mbegu au tawi lililopandwa. Baadhi ya mimea hutoa natija kwa mwanadamu ilhali mingine kama vile magugu hutoa hasara. Katika tamthilia ya *Zilizala* pana mimea na matunda yao ambayo imetumiwa kitaashira. Mkungu huweza kuwa nomino inayorejelea suke la ndizi zilizojishika kwenye mkole ambapo ndizi zimejipanga katika vichane kadhaa. Ndizi ni tunda la mgomba. Ndizi huweza kuliwa ikiwa mbivu bila kupikwa na wakati mwingine hupikwa na kutengeza chakula cha 'matoke'. Hivyo, ndizi ni suluhu ya baa la njaa katika mataifa mengi barani Afrika. Katika *Zilizala*, mkungu ni taashira ya uhuru. Hii ni kwa sababu huwa na matunda ambayo watu hutoa jasho jingi wakipanda, kurutubisha na hata kupalilia. Kupalilia ni kuondoa magugu kwenye shamba la mazao kwa jembe au kung'oa kwa mkono (Tuki 2013). Katika tamthilia hii, kupalilia ni taashira ya vita vya uhuru vinavyoendelezwa na Waafrika wazalendo. Upaliliaji wenyewe ni mwafaka maadamu hatimaye migomba itaweza kuzaa mikungu mikubwa ya matunda ndizi.

Magugu ni majani yasiyohitajika kwenye shamba. Pia huitwa kwekwe. Kwekwe zikienea shambani huzalisha hasara kubwa. Hii ni kwa sababu magugu hufyonza virutubishi vyote mle shambani na hivyo kusababisha ukuaji wa mimea dhoofu na isiyo na mazao bora au isiyo na mazao yoyote. Kitaashira, magugu ni taashira za viongozi dhalimu hasa katika mataifa maskini ya Kiafrika. Kwa upande mwingine, vimelea na kwekwe ni taashira za viongozi wa mataifa tajiri ambayo hunawiri kwa kunyonya mataifa yanayoinuka kupitia uchumi, siasa na hata masuala ya kijamii. Ni mataifa ambayo huchangia vita vya wenyewe kwa wenyewe kwa mfano, barani Afrika kwa lengo la kupata soko la ala za vita yanazozitengeneza kwa wingi.

**Taashira ya Miundomsingi**

Kuhusu miundomsingi, majengo yametumika kama taashira. Jengo moja lililotumika kitaashira ni kibanda cha nguruwe. Kibanda ni nyumba ndogo inayotumiwa kwa shughuli maalumu, kwa mfano, kufugia nguruwe au hata kuku. Pia huweza kuwa nyumba ndogo wanapoishi watu wa kipato cha chini zinazopatikana maeneo ya mashambani au mijini. Vibanda huweza kupatikana

katika janibu zenye msongamano mkubwa wa watu wenye uwezo finyu wa kiuchumi. Msongamano huu huchangia uchafu kuzagaa popote na njia kubanwa sana au hata kukosekana kabisa. Kwa upande mwingine, nguruwe ni mnyama anayefugwa, mnene na mwenye pua kubwa. Hivyo basi, mara nyingi kibanda cha nguruwe huwa na uvundo mkali, ambao huzalishwa na uchafu pamoja na kinyesi na mikojo ya nguruwe. Aidha, hujengwa kwa mawe futi tatu kutoka chini na kisha huzingirwa na nyavu zenye matundu kuruhusu hewa kupenya kwa urahisi. Hatimaye huezekwa mabati juu kuzuia mvua na jua kali. Ikizingatiwa kwamba nguruwe hula chakula chochote bila kubagua, mivuke ambayo hutoka kwenye kibanda huwa haielezeki wala kumithilishwa.

Katika *Zilizala*, pana kibanda cha nguruwe anapofanyia kazi mhusika Puma. Puma anafanya kazi kwa bepari Memetuka. Hii ni taashira ya baadhi ya mataifa ya ulimwengu, hususan barani Afrika ambapo ufisadi unavunda. Ufukara, ukosefu wa ajira, unywaji wa pombe haramu, matumizi ya dawa za kulevya, uharibifu wa mazingira, ukosefu wa elimu bora, kudorora kwa usalama na dhiki pamoja na changamoto nyingine nyingi ni masuala mengine ambayo yanaongeza uvundo katika kibanda cha nguruwe, yaani mataifa yanayozama katika maovu.

Hali hii ni mithili ya ile inayoangazwa na Ayi Kwei Armah katika *The Beautyful Ones Are Not Yet Born.* Katika kazi hii, choo kichafu cha umma kimetumika kama taashira ya uchafu wa ufisadi uliokita katika baadhi ya mataifa ya Afrika. Pia kibandani mwa nguruwe mna pingu zinazotajwa na Udenda ambazo ni taashira za utumwa ulimwenguni hasa katika mataifa yaliyo na uongozi mbaya. Pana mataifa ulimwenguni, na hata katika bara la Afrika ambayo yangali katika minyororo ya utumwa wa kiuchumi, kisiasa na kijamii unaosababishwa na viongozi Waafrika. Katika *Zilizala* Memetuka anawakilisha viongozi dhalimu, ilhali Puma anawakilisha wananchi fukara katika mataifa mengi barani Afrika.

Kibanda cha nguruwe kimekuwa na athari kwa Puma anayefanya kazi huko. Memetuka, kwa mfano, anashangazwa na mabadiliko ya Puma. Analalamika kwamba zamani angemwambia abweke, angebweka, lakini mambo yamebadilika. Hili linaashiria athari za kibanda cha nguruwe. Jinsi nguruwe wanavyozoea kuinama na kutii bila kuuliza swali, ndivyo Puma alivyokuwa kwa mwajiri wake Memetuka. Aidha, mawazo yake hayakuwa na tofauti kubwa na yale ya nguruwe hadi alipoamua kuosha kibanda cha nguruwe. Usafishaji huu ni taashira ya kubadili mawazo na nia. Mawazo ya Puma yanapata uhuru na wazo la kununua shamba linamvaa. Wazo hili linamghadhabisha Memetuka kwa sababu angependa Puma aendelee kuwa mtumwa wake. Angependa Puma aendelee kudumisha uchafu na uvundo, na kupalilia ufisadi na utumwa katika kibanda cha nguruwe. Hili linaashiria viongozi wanaonyanyasa raia, na ambao hawangependa watu wazindukane wasije wakataka kuacha utumwa wao wa mawazo kama anavyofanya Puma. Utumwa kama huu huwasaidia wanasiasa kujipigia upatu wakati wa kampeni. Hii ndiyo sababu Memetuka anamtishia maisha na kusema anaweza kumtia pingu.

**Taashira ya Ala**

Mtunzi ametumia ala mbalimbali kitaashira. Mfano mzuri ni nyavu zinazopatikana katika *Zilizala*. Wavu ni nyuzi au nyaya zilizosukwa na kufanya utandu wenye tundu ndogondogo unaotumiwa kwa shughuli mbalimbali kama vile; uvuvi, kutegea wanyama, kutegea watu, kufunga kwenye magoli. Aidha huitwa kimia. Wavu kwa wingi huwa nyavu na mwandishi Kimani Njogu amelitumia neno hili kitaashira. Katika *Zilizala*, nyavu ni taashira ya mali ya umma. Badala ya Udenda kuchunga na kulinda mali ya umma, yeye anayavunja bila simile. Kumba anadai kuwa Udenda anapiga nyavu mkwaju na kuzipasua. Anaongeza kuwa hii ni tabia yake tangu awe mtoto. Ikizingatiwa kuwa baadhi ya makabwela hutafuta riziki kwa kunasa samaki kupitia nyavu, kitendo cha Udenda bila shaka kinatinga uwezo wa maskini kujiambulia chakula. Aidha, nyavu ni taashira ya watu ambao Udenda alinyanyasa tangu utotoni. Ndiposa Kumba anadai kwamba alianza kupasua nyavu wakati huo, yamkinika kuhujumu wasichana kimapenzi. Taashira hii inadhihirika wakati Udenda anacheka kutokana na lawama hizi, badala ya kukasirika.

Majembe ni wingi wa neno jembe. Jembe ni kifaa cha kulimia chenye umbo bapa kilichotengenezwa kwa chuma ambacho kina makali upande mmoja na upande mwingine una tundu ambamo hutiwa mpini. Kando na kulima, jembe huweza kutumika katika kupalilia mashamba. Shoka nacho ni kifaa kilichotengenezwa kwa chuma na ambacho hutiwa makali na chenye mpini na hutumiwa kwa kupasulia kuni au kukatia miti. Katika *Zilizala*, majembe na mashoka ni taashira za silaha za kipigana na ufukara, ukame na njaa barani katika mataifa maskini. Hii ni kwa sababu tofauti na wakulima matajiri ambao wanaweza kutumia mashine kama vile trekta katika kilimo, maskini hawana huo uwezo. Badala yake humenyeka kwa kutumia nguvu zao wanaposhika mashoka na majembe na kutoa jasho ili wapate riziki. Hivyo, vifaa hivi ni taashira ya juhudi za watu maskini wanaotumia pembejeo zinazohitaji nguvu mradi wajipatie riziki. Hata hivyo, ala hizi bado ni taashira ya silaha ya ukombozi kama unaodhihirishwa na vita katika *Sudana.* Maskini, tofauti na matajiri, hawana silaha za vita kama vile bastola, lakini wanatumia mikuki na mapanga kupigana na Wamerope.

Ala nyingine iliyotumika kitaashira katika *Zilizala* ni bahasha. Lundo la bahasha ni mkusanyiko wa vifurushi au mifuko mingi pamoja iliyotengenezwa kwa njia maalumu na inayotumiwa kutumia barua au ujumbe ulioandikwa katika karatasi. Nchini Kenya, neno ‘bahasha’ aghalabu hutumiwa kuashiria rushwa. Lundo la bahasha lililo mezani katika afisi ya Udenda ni taashira ya ufisadi. Katika afisi hii, tunaelezwa kuwa pana inspekta aliyevaa sare yake na kifimbo mkononi. Kando yake penye meza pana lundo la bahasha. Bahasha hii inawakilisha rushwa inayoliwa na walinda usalama na kulemaza juhudi za kuimarisha nguzo za haki na ukweli katika baadhi ya mataifa duniani.

Isitoshe, marundo haya ya bahasha yanadhihirisha kuwa Udenda ni kiongozi wa kupokea bahasha, na hivyo ni fisadi. Ufisadi wake umelindwa na inspekta wa polisi,

suala ambalo ni kinaya. Isitoshe, Udenda analindwa na katiba iliyofurika vifungu vinavyoruhusu utoaji na upokeaji wa rushwa. Viongozi wamenyofoa katiba na kuibadili hapa na pale ili kuhalalisha ufisadi, na hivyo kujisetiri na mashtaka. Ndiposa Udenda hana fedheha anapoonyesha lile lundo la bahasha ofisini mwake kana kwamba ni jambo la kawaida. Mathalani, kuna kifungu kinachoruhusu utoaji wa hongo kwa asilimia mia moja. Udenda anakitaja kifungu HO/NGO/1/99 cha uwezo wa Diwani. Silabi HO na NGO zikishikanishwa zinaunda neno moja ambalo ni hongo. Hili linadhihirisha kwamba hongo imeidhinishwa na sheria zilizopo. Lakini Udenda haungami kuwa hizi ni hongo bali anadai ni zawadi kutoka kwa watu walioridhika na kazi zake.

Kifungu hiki ni kigeni kwa inspekta na hakika anashangaa kukisikia kwa mara ya kwanza. Kinaya ni kuwa, kwa mujibu wa Udenda, kifungu hicho kiliongezwa wakati wa kusherehekea uhuru kwa ajili ya kuelewa maana ya uhuru kikamilifu. Hiki ni kinyume cha matarajio, kwa sababu hongo huharibu uchumi wa taifa kwa kiwango kikubwa. Aidha, ufisadi ni donda sugu linalohitaji ushirikiano wa kila mja; wazee kwa vijana, wake kwa waume, tajiri kwa maskini, mlemavu na asiye mlemavu alimradi kila mja ili kuliganga.

**Hitimisho**

Makala haya yamejadili matumizi na uamilifu wa taashira katika tamthilia za *Zilizala* na *Sudana*. Yamefanya hivyo kupita mambo kadha wa kadha yaliyotumiwa kujenga taashira hizi. Haya ni pamoja na vyombo vya usafiri, miundomsingi, hali za maumbile na ala mbalimbali. Yameonyesha kuwa waandishi wametumia mbinu hii kwa ajili ya kusawiri mambo mengi mazito. Kimsingi, taashira imetumika kuangaza ukoloni mamboleo unaoitwa utandawazi kitasfida. Katika ukoloni huu, imedhihirishwa kuwa mataifa yenye nguvu huzidi kujiongezea nguvu kwa kunyonya jasho na rasilmali za mataifa yanayoinuka kiuchumi. Kufanikisha uovu huu, mabepari katika mataifa ya kigeni hutumia vibarakala wao ambao aghalabu huwa ni viongozi katika mataifa yanayochipuka. Lakini makala haya yamebaini kuwa hakuna refu lisilokuwa na ncha maadamu baada ya wateswa wengi kuhangaishwa sana, hatimaye hutaka mabadiliko chanya. Hapa hudai haki zao kwa njia nyingi, ikiwemo ile ya ncha ya upanga inayopindua tawala zilizopo kama ilivyobainika katika *Zilizala* na *Sudana.*

**Marejeleo**

Armah, A. K. (1984). *The Beautyful Ones Are Not Yet Born*. London: Heinemann.

Cope, B. na Kalantzis, M. (2000). *Multiliteracies: Literacy Leaning and the Design of Social Features.* London: Routledge.

Katola, K. E. (2006). *Ishara Zinazotumiwa Kudhalilisha Wahusika wa Kike katika Tamthilia za Kiswahili Nne.* Tasnifu ya Shahada ya Uzamili katika Chuo Kikuu cha Nairobi.

Khamis, S. A. M. (2004). *Images of Love in the Swahili Taarab Lyric: Local Aspects and Global Influence.* Nordic Journal of African Studies 13(1), 30 – 64.

Kilanga, B. S. (2014). *Ishara katika Kaptula la Marx na Kijiba cha Moyo: Mtazamo wa Kisemiotiki.* Tasnifu ya Shahada ya Uzamili katika Chuo Kikuu cha Nairobi.

Mazrui, A. M. na Njogu, K. (2006). *Sudana*. Nairobi: Longhorn Publishers.

Mazrui, A. M. na Syambo, B. K. (1992). *Uchambuzi wa Fasihi.* Nairobi: East African Educational Publishers.

Mbatiah, M. (2001). *Kamusi ya Fasihi*. Nairobi: Standard Text Books and Publishing.

Njogu, K. (2006). *Zilizala*. Nairobi: Longman Kenya Ltd.

Njogu, K. na Chimerah, R. (1999). *Ufundishaji wa Fasihi Nadharia na Mbinu.* Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation Ltd.

Onyango, J. O. (2011). Imagery as a Pervasive Feature of Style: The Case of Ebrahim

Hussein's Mashetani (1971). In Makokha TKS, Kahaji, E., & Dipio, D. (Eds.), *In East African Literature: Essays on Written and Oral Traditions (pp. 399 – 414)* . Logus Verlag Berlin.

Ntarangwi, M. (2004).*Uhakiki wa kazi za fasihi*. Rock Islands.Augustine college.

Wamitila, K.W. (2002). *Uhakiki wa Fasihi Misingi na Vipengele Vyake.* Nairobi: Phoenix Pubishers Ltd.

Wamitila, K.W. (2003). *Kamusi ya Fasihi; Istilahi na Nadharia*. Nairobi: Focus Publications Ltd.

Wamitila, K.W. (2010). *Kanzi ya Fasihi 1: Misingi ya Uchanganuzi wa Fasihi.* Nairobi: Vide-Muwa Publisher.